

VIELELEZO VINAVYOHITAJIKA WAKATI WA UJAZAJI WA FOMU YA MAOMBI YA ETD

Vielelezo vya Lazima

- 1. Cheti cha kuzaliwa Mwombaji
- 2. Cheti/Kiapo cha kuzaliwa Mzazi wa Mwombaji
- 3. Kitambulisho cha Taifa
- 4. Picha ya Mwombaji ya hivi karibuni yeye kivuli cha rangi ya nyeupe isiyokoza (White Background)
- 5. Ada ya Ombi ni Tsh. 20,000/= au \$ 20 USD

Vielelezo vya ziada

- 1. Leseni, Pasipoti, NIDA, Zan ID
- 2. Barua ya kutoka Serikali ya Mtaa/Mwajiri
- 3. Ushahidi wa safari au Ushahidi wa Shughuli anayofanya Mwombaji

JINSI YA KUJAZA FOMU YA MAOMBI YA ETD

- 1. Tembelea tovuti ya Uhamiaji (www.immigration.go.tz) na kisha chagua online etd application, au tembelea moja kwa moja linki ifuatayo: etdonline.immigration.go.tz na kisha kuendelea na maombi ya Hati ya Dharura ya kusafiria.
- 2. Karatasi inayokubalika kuchapa ETD ni yenye ukubwa wa A4 (**yaani A4 size**) na iwe na rangi nyeupe. Aidha, uzito wa karatasi unapaswa kuwa **gram 80** (yaani karatasi ya kawaida ya A4). Pia, Mwombaji anatakiwa kuchapisha kwa kutumia maandishi yenye rangi (**Colored printing**).
- 3. Hati ya Dharura inabidi ichapwe kwenye karatasi moja yenye kurasa mbili. Kurasa ya mbele iwe na taarifa za mwombaji na kurasa ya pili iwe neno Visa
- 3. Bofya Ombi jipya kuanza ombi kwa mara ya kwanza
- 4. Bofya ENDELEA ili kuendelea na Ombi ambalo halikufikia mwisho. Utahitajika kujaza Namba ya Ombi na barua pepe yako
- 5. Jaza Taarifa zako sahihi kwa ukamilifu
- 6. Hifadhi Namba yako ya Utambulisho (Application ID) kwa matumizi ya baadaye.
- 7. Jaza taarifa za ETD ya zamani (Kama umewahi kuwa na ETD)
- 8. Jaza taarifa za wadhamini na watu ambao ungependa wapewe taarifa endapo utapata tatizo lolote
- 9. Ambatanisha vielelezo vyote vinavyohitajika kwa kuzingatia maelekezo
- 10. Hakiki taarifa zako zote na kisha bofya kukubaliana nazo ikiwa ziko sahihi.
- 11. Lipia ombi lako baada ya kupatiwa namba ya kumbukumbu ya malipo (Control Number).
- 12. Kitufe cha kufuatilia Hali (Status) ya Ombi kinakuwezesha kufuatilia Ombi lako limefikia hatua gani .
- 13. kwa mwombaji atakayeomba kwa kutumia NIDA yake au Mdhamini atatakiwa kuchapisha fomu yake na kuiwasilisha ofisi ya Uhamiaji .
- 14. Kwa mwombaji anaye omba kwa kutumia pasipoti yangu au kuhuisha (Renew) baada ya kulipia atachapisha hati yake ya kusafiria na kwa mwombaji wa NIDA au aliyedhaminiwa Baada ya ombi kufanyiwa kazi ofisi ya Uhamiaji (assessment na Approval) atachapisha Hati yake ya Kusafiria na nakala ya hati ya dharura itatumwa kwenye barua pepe yake.